***8. Nini nia na umuhimu wa sheria zinazohusiana na mgongano wa maslahi***

Umuhimu wa Sheria hizi ni kuwa zinaainisha mambo na mienendo ambayo inasababisha mgongano wa maslahi ili kuwawezesha viongozi wa umma kutambua, kubaini, kufichua na kupanga mambo yao katika namna ambayo inazuia mgongano kati ya maslahi binafsi ya kiongozi na maslahi ya umma kutokea. Lengo la kulipa uzito na kulisimamia kwa karibu suala hili la mgongano wa maslahi ni pamoja na: (i) Kuimarisha imani ya wananchi kwa uongozi wa nchi na utendaji kazi wa Sekta ya Umma; (ii) Kujenga dhana kuwa maamuzi yanayotolewa na viongozi wa umma hayakushawishiwa visivyo, kwani Mgongano wa maslahi unatishia ubora wa maamuzi na pia kuyafanya maamuzi yenyewe yasiaminike na mwananchi; na (iii) Kuimarisha uhalali (legitimacy) wa Taasisi na maamuzi yanayotolewa.

***9. Je? Kuna sababu yoyote ya kuchukua hatua kuhusu hisia za uwepo wa mgongano wa maslahi***

Ndiyo, upo umuhimu wa kuchukuliwa hatua kunapoonekana kuwepo kwa hisia za uwepo wa mgongano wa maslahi, kwa kuwa zipo athari hasi za kutochukuliwa kwa hatua kutokana na hisia hizo. Kwani hali hiyo ya hisia ikiachwa inaweza kuathiri imani waliyonayo wananchi kuhusu uadilifu wa viongozi wa umma na mchakato mzima wa kufanya maamuzi.

***10. Je? Kiongozi wa umma anatakiwa kutamka mgongano wa maslahi hata ambapo hakuna manufaa ya kifedha aliyoyapata ama upotevu uliotokea.***

Ndiyo, mgongano wa maslahi si lazima ujitokeze tu pale kunapokuwepo na maslahi ya kifedha au upotevu, yapo pia manufaa yasiyo ya kifedha yanayoweza kumuingiza kiongozi katika mgongano wa maslahi hasa katika mazingira ya uhusiano wa kidugu au urafiki, vikundi vya kijamii, vyama vya ushirika nk kwa kuvisaidia kwa namna yoyoye kwa kutumia wadhifa wake kwa upendeleo ambapo baadae anaweza kupata manufaa ya kijamii kutoka kwa washirika au vikundi hivyo.

***11. Je? inawezekana kuzuia mgongano wa maslahi***

Kiongozi au Mtumishi wa Umma anaweza kuzuia mgongano wa maslahi kwa kupanga mambo yake kwa namna ambayo itazuia mgongano kati ya maslahi yake binafsi na maslahi ya umma kutokea. Njia nyingine ni pamoja na: kufanya uamuzi kwa kuzingatia sheria, kanuni na tarartibu, kutoa taarifa hadharani kuhusu maslahi binafsi katika suala linalofanyiwa kazi au uamuzi, Kujiuzulu katika wadhifa unaosababisha mgongano wa maslahi, kujitoa (recusal) kushiriki katika utekelezaji au kufanya uamuzi kwenye jambo ambalo ana maslahi binafsi na kuachia maslahi binafsi yanayosababisha mgongano wa maslahi kutokea .

***12. Wapi ninaweza kupata Sheria zinazosimamia masuala ya mgongano wa maslahi***

Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Na. 13 ya mwaka 1995 inapatikana Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma na katika Tovuti ya Sekretarieti ambayo ni: www.maadili.go.tz.

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA RAIS

## SEKRETARIETI YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA

# MASWALI NA MAJIBU MUHIMU KUHUSU MGONGANO WA MASLAHI

***1. Nitajuaje kama nina Mgongano wa Maslahi?***

Ili kuwe na mgongano wa maslahi kunatakiwa kuwe na mambo manne: Maslahi ya msingi, maslahi ya umma au maslahi ya taaluma; Maslahi ya pembeni au binafsi;Jukumu au wajibu kwa umma; na Mgongano kati ya maslahi binafsi na maslahi ya umma katika utekelezaji wa jukumu au wajibu kwa umma. Maslahi binafsi maana yake ni njia binafsi za kiuchumi au zisizo za kiuchumi za kiongozi au mtumishi wa umma ambazo zinaweza kumshawishi kufanya uamuzi wa upendeleo katika utekelezaji wa majukumu ya umma.

***2. Je, ni kosa kuwa na mgongano wa maslahi?***

Siyo kosa kwa kiongozi kuwa na maslahi binafsi. Lakini ikitokea kuwa maslahi hayo yanakinzana ama kugongana na majukumu yake kwa umma ni lazima yadhibitiwe inavyotakiwa kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu. Mgongano hautokei kwa sababu tu kiongozi anayo maslahi binafsi nje ya majukumu yake kwa umma. Taratibu za kudhibiti mgongano wa maslahi zikikiukwa na kusababisha athari katika maamuzi au utekelezaji wa kazi za umma ndipo kosa linapodhihiri.

***3. Je, Jukumu la Kiongozi ni nini katika kudhibiti mgongano wa maslahi?***

Kila inapowezekana, Kiongozi wa Umma anapaswa kujiepusha na mgongano kati ya maslahi yake binafsi na maslahi ya umma kwa kupanga mambo yake katika namna ambayo itazuia mgongano kutokea. Endapo utatokea mgongano kati ya maslahi binafsi ya kiongozi au mtumishi wa umma na maslahi ya umma, anao wajibu wa kubaini na kudhibiti mgongano wa maslahi uliojitokeza kwa kuweka mbele maslahi ya umma kwa kufuata taratibu zilizowekwa na sheria au kwa kushauriana na mamlaka zilizopo kisheria.

***4. Je, ni jambo jema kukaa kimya bila kutoa taarifa ya mgongano wa maslahi?***

HAPANA. Ni vizuri mgongano wa maslahi ukabainishwa na kufichuliwa mapema ili udhibitiwe kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa kwa mujibu wa sheria na kanuni. Endapo kiongozi atabaini mgongano wa maslahi na kushindwa kutamka kwa mujibu wa taratibu zilizopo inaweza kuhatarisha uadilifu wa Kiongozi husika na kuonekana kuwa amekiuka maadili ya Viongozi wa Umma, hivyo kulazimika kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria. Iwapo Kiongozi hana uhakika wa uwepo wa mgongano wa maslahi katika jambo analotekeleza au kulitolea uamuzi, anashauriwa kutafuta ushauri mapema kwa wakuu wake wa kazi au kwa Ofisi ya Kamishna wa Maadili ya Viongozi wa Umma.

***5. Je, ni makosa kukubali kupokea fadhila ya chakula ama zawadi kutoka kwa mkandarasi au mdau yeyote ambaye huwa anafanya biashara/shughuli zake na Taasisi yetu?***

Kiongozi anashauriwa ajiepushe kuomba au kupokea fadhila kama vyakula na zawadi nyingine ambazo zinagharamiwa na watu ambao wanafanya biashara au kazi na Taasisi yake kinyume na utaratibu uliopo kisheria. Hii ni muhimu kwa sababu watu wanaoingia gharama hizo kwa ajili ya kiongozi wa umma wanaweza kuwa na malengo yao ambayo kwa namna moja ama nyingine yanaweza kumshawishi kiongozi wa umma kutekeleza wajibu wake au kutoa maamuzi kwa upendeleo kwa mtu aliyemfadhili. Kiongozi akihitaji huduma ya chakula ama vinginevyo, akiwa kwenye shughuli ya umma ni lazima alipie mwenyewe kwa gharama zake na ataenda kuomba kurejeshewa fedha zake kutoka kwa mwajiri wake kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za ofisi yake.

***6. Je, ni adhabu gani zinazoweza kutolewa kwa kujihusisha na mgongano wa maslahi***

Ikithibitika kiongozi amejihusisha kwenye migongano ya maslahi ni kosa la kimaadili, hivyo adhabu zake ni kama zilivyoainishwa kwenye Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Na. 13 ya mwaka 1995. Adhabu hizo ni pamoja na: i) Kuonywa na kupewa tahadhari; ii) Kushushwa cheo; iii) Kusimamishwa kazi; iv) Kufukuzwa kazi; v) Kuchukuliwa hatua za kinidhamu kwa mujibu wa Sheria za nchi zilizopo; vi) Kushauriwa ajiuzulu wadhifa alionao; na vii) Kupewa adhabu nyingine zinazoruhusiwa kwa mujibu wa Sheria za nchi.

***7. Je, ni hatua zipi za kuchukua ninapobaini uwepo wa mgongano wa maslahi?***

Mara kiongozi au mtumishi wa umma anapotambua kuwa anao mgongano wa maslahi, kwa kuzingatia matakwa ya Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo iliyopo, kiongozi au mtumishi huyo atahitajika kutoa tamko rasmi la mgongano wa maslahi kwa mujibu wa Sheria na utaratibu uliooainishwa katika Kanuni za Kudhibiti Mgongano wa Maslahi, na kuliwasilisha kwa mamlaka zinazohusika. Kiongozi au mtumishi wa umma anaweza kulazimika kutoa tamko la maneno anapokuwa kwenye mikutano au vikao. Hata hivyo, anapaswa kuhakikisha kuwa taarifa hizo anazozitoa kwa maneno, zinaingizwa kwenye kumbu kumbu sahihi za vikao. Daima ni bora zaidi kwa kiongozi au mtumishi wa umma kuwa muwazi kutamka na kuelekezwa namna ya kudhibiti  mgongano wa maslahi badala ya kuficha jambo hilo.